



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA
MITAA
HALMASHAURI YA MJI WA KOROGWE**



Mtaa wa Majengo, Barabara ya Moshi, S. L. P. 615 Korogwe –Tanga, Simu: 027-2650050

Nukushi: 027- 2650075 Barua Pepe: info@korogwetc.go.tz Tovuti:

www.korogwetc.go.tz

Kumb.Na. HMK/C.5/03/15

17/11/2025

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri (M) Korogwe anawatangazia Watanzania wenye sifa kuomba nafasi saba (7) za kazi katika Halmashauri hii baada ya kupata kibali kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mchanganuo ufuatao:-

1.1. MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II – NAFASI 3

1.1.1. MAJUKUMU NA KAZI

- i. Kuorodhesha barua zinazolingia masjala kwenye rejista (Incoming correspondence register);
- ii. Kuorodhesha barua zinazotoka nje ya taasisi kwenye rejista (outgoing corresponding register);
- iii. Kusambaza majadala kwa watendaji (action officers);
- iv. Kupokea majalada yanayorudi masjala kutoka kwa watendaji;
- iv. Kutafuta kumbukumbu/nyaraka/majalada yanayohitajika na watendaji;
- v. Kurudisha majalada kwenye shubaka/kabati la majalada (racks/filing cabinets); na
- vi. Kufuatilia mzunguko wa majalada ndani ya Taasisi (File tracking)

1.1.2. SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa mwenye Elimu ya kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Stashahada/Diploma (NTA Level 6) katika fani ya Utunzaji wa Kumbukumbu kutoka vyuo vinavyotambuliwa na serikali, wenye ujuzi wa

kutumia kompyuta.

1.1.3. NGAZI YA MSHAHARA

TGS C

1.2. DEREVA DARAJA LA II – NAFASI 4

1.2.1. SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wenye cheti cha Kidato cha Nne (Form IV) na Leseni ya Daraja E au C ya uendeshaji magari ambayo wamefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali pamoja na vyeti vya mafunzo vilivyowapatia sifa ya kupata madaraja husika. Wawe wamehudhuria mafunzo ya msingi ya Uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha VETA au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.

1.2.2. KAZI NA MAJUKUMU

- i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari;
- ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
- iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari
- iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- iv. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari
- v. Kufanya usafi wa gari na
- vi. Kufanya kazi nyingine kadiri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake.

1.2.3. NGAZI YA MSHAHARA

TGS B

MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI

- i. Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- ii. Waombaji wenye ulemavu wanahamasishwa kutuma maombi na wanapaswa kuainisha kwenye Mfumo wa kuombea ajira ulemavu walionao kwa ajili ya taarifa kwa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;

- iii. Waombaji kazi wa kada ya Dereva Daraja la II wenye leseni Daraja E au C wanapaswa KUAMBATISHA vyeti vya mafunzo ya Udereva vilivyowapatia sifa ya kupata madaraja husika.
- iv. Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (Detail Curriculum Vitae) yenye anuani inayotumika, namba za simu zinazopatikana na Anuani ya Barua Pepe (E-mail address) pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika.
- v. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka **Na. CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.**
- vi. Maombi yote yaambatane na vyeti vya Elimu naTaaluma vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya Kidato cha Nne au Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika. **Postgraduate/ Degree/ Advanced Diploma/ Diploma/ Certificates, - Cheti cha mtihani wa Kidato cha IV na VI, - Computer Certificate, -Vyeti vya Kitaaluma (Professional Certificate from Respective Boards).**
- vii. "Testimonial ", "Provisional Results ", "Statement of results ", hati ya matokeo ya Kidato cha Nne na Kidato cha Sita **(FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**
- viii. Waombaji waliosoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na vimethibitishwa na Mamlaka husika **(TCU, NECTA na NACTE).**
- ix. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wanakibali kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi;
- x. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

xi. Mwisho wakutuma maombi ya kazi ni tarehe **30 Novemba, 2025.**

xii. **MUHIMU:** Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu, anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa:-

Mkurugenzi wa Mji,
Halmashauri ya Mji Korogwe,
1 Mtaa wa Halmashauri,
S.L.P. 615,
21268 Korogwe.

xiii. Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa Kielekroniki wa Ajira **(Recruitment Portal)** kupitia anuani ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa “Recruitment Portal”.

Tangazo hili limetolewa na;

**MKURUGENZI WA MJI
HALMASHAURI YA MJI WA KOROGWE**